TANGAZO LA SERIKALI NA. 239 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA SALAWE YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Salawe ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

*Tangazo la Serikali Na. 239 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*
Eneo la urasimishaji lipo ndani ya Mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 484658.776MS, 9639011.662KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KZ85º59'41.66''MG kwa umbali wa kilometa 1.86 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 486616.604MS, 9638874.582KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KZ24º50'32.56''MG kwa umbali wa kilometa 0.851 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 487016.445MS, 9638010.924KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KZ01º59'19.62''MG kwa umbali wa kilometa 2.197 hadi kwenye alama ya mpaka ya upiamji namba D yenye majira - nukta 486936.726MS, 9635715.165KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KZ89º51'13.62''MS kwa umbali wa kilometa 2.226 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 484610.435MS, 9635709.228KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ00º50'19.07''MG kwa umbali wa kilometa 3.302 hadi ulipoanzia.

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*